

## Udhibiti mkali wa wadudu hupunguza uharibifu

Udhibiti mkali wa wadudu ili kukinga wadudu na magonjwa huhitaji aina zinazostahili, kunyunyizia kunakohitajika, kuwadhibiti maadui wa kawaida na kutumia vifaa vya kupanda mapema, matumizi ya viua dudu vilivyochaguliwa, na utoaji wa vitu visivyokuwa na athari.



Pilipili



Mexican Marigold

## Tumia majani yaliyoboreshwa ili kuimarisha sehemu kavu zilizoharibiwa

Majani aina ya '*Cenchrus ciliaris*' yamebuniwa na kusambazwa katika sehemu zenye mvua chache. Zaidi ya majani kwa wanyama, nyasi hiyo huimarisha sehemu zilizoharibiwa na hivyo kuchangia katika uhifadhi wa mazingira.



Ng'ombe wakila malisho yaliyoimarishwa



### Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

### Watayarishaji:

Odongo, O. M., Kiiya, W., Mutoko, M. C., Mulaa, M.A., Wambani, H. N.  
na Nyambati, E. M.

### Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

### Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Kitale

S.L.P. 450 Kitale, 30200

Simu: 054 201079

Nukulishi: 054 30378

Baruapepe: inmakt@africaonline.co.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 76 /2008

**Shilingi 20 za Kenya**

## Hifadhi afya ya mazingira kwa kutumia teknolojia zilizothibitishwa na KARI



## Utangulizi


Maazimio ya KARI ni kuchangia katika kuimarisha maisha kupitia njia zilizobuniwa za kilimo pamoja na weledi. Katika kutekeleza maazimio haya, athari mbaya katika mazingira inakwepwa ili kuhakikisha kilimo ambacho chaweza kudumishwa.

## Jinsi KARI inavyochangia uhifadhi wa mazingira

KARI hufanya utafiti wa mimea yenye mazao ya juu, jinsi ya kuwadhibiti wadudu na virutubishi, ukakamavu wa mimea inayohitajika uchanjaji wa mifugo n.k. katika maeneo tofauti tofauti na mitindo tofauti ya kilimo humu nchini.

## Mimea yenye mazao ya juu huhitaji ardhi ndogo

Mimea yenye mazao ya juu katika nyanda za juu, maeneo ya upoteaji wa mvuke yametayarishwa na kufahamishwa. Kwa mfano, Sampuli ya mahindi ya KH 600 – I ID yenye kiwango takriban ngunia 40 kwa kila ekari ikilinganishwa na ngunia 10 kutoka kwa aina za kawaida.



**Mahindi yenye mazao ya juu**

Nyasi za kigeni za ng'ombe zinaweza kuzaa kati ya tani 8 na 10 kwa kila ekari kwa kupanda aina ya 'Bana'



**Nyasi ya kigeni (Napier) yenye mazao mengi**

badala ya tani 2 hadi 4 kwa ekari ya majani kavu yanayopatikana kutoka kwa majani ya kawaida. Aina ya mimea inayotoa mazao mengi huhitaji eneo ndogo ikilinganishwa na ile inayotoa mazao madogo. Hii husababisha kupunguza shindikizo katika shamba na kuzuia chemchemi za maji kuharibiwa.

## Aina zinazostahimili wadudu na magonjwa zinahitaji kemikali kiasi kidogo

Mazao yanayoweza kustahimili magonjwa kama vile viazi vya Tigoni na maharagwe aina ya KK 8 yametolewa na KARI. Viazi hivyo vinastahimili ugonjwa wa baridi na maharagwe inastahimili kuoza kwa mizizi.

## Teknolojia ya kuvuta na kusukuma wadudu

Ndizi zinazolishwa kwa mtindo wa kisasa zinahitaji kemikali chache na hutupatia funiko la mchanga.




**Mimea tofauti katika teknolojia ya kuvuta - kusukuma**

Uzalishaji wa haraka wa ndizi kwa kutumia mtindo wa Sayansi ya kisasa umethibitishwa na kuenezwa na KARI. Ndizi hizi haziambukizwi magonjwa wala kuathiriwa na wadudu. Hivyo, zinahitaji kemikali kiasi kidogo. Ndizi ni zao la kila msimu mwakani na huzuia mmonyo wa udongo.

## Mbolea ya kijani kibichi huboresha rutuba ya mchanga na kusafisha hewa

Mbolea kutoka kwa jamii ya kunde kama vile maharagwe aina ya *mucuna* huboresha rutuba ya mchanga na maumbo yake. Majani yake makubwa hupunguza mmomonyoko wa udongo na kufanikisha mimea ya mchanga. Mimea hii ya mwaka wote hupunguza kiwango cha dioksidi ya kaboni katika hewa na hivyo kupunguza joto ridi la dunia.

Majani ya *mucuna* yana asilimia 17 ya protini na yanapolishwa ng'ombe mapato ya maziwa huongezeka. Yanaweza kutengenezwa chakula cha mifugo kwa kuchanganya na mahindi kwa kiasi cha 75% mahindi na 25% *mucuna*.



**Mucuna**